


# UBABEDUME KATIKA TAMTHILIA YA *BEMBEA YA MAISHA* (2022)

*Musyimi D. M. and Nyagah S. K.*
*Chuo Kikuu Cha Chuka, Kenya*
*musyimidorcas@yahoo.com*
dmusyimi@chuka.ac.ke

**Musyimi D. M. and Nyagah S. K.(2023) Ubabedume katika tamthilia ya bembea ya maisha In: Isutsa, D. K. (Ed.). Proceedings of the Chuka University 8th Annual International Research Conference held in Chuka University, Chuka, Kenya from 24th to 25th November, 2022. 218-223 pp.**

## IKISIRI

Mfumo-dume humpa thamani kubwa mwanamume huku ukimdhalilisha mwanamke kwa sababu ya jinsia yake. Imani hii dunishi imo katika itikadi na tamaduni zinazohimiliwa na mfumo wa muundo wa kijamii ambao mwanamume anapewa nguvu na uwezo zaidi dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za maisha hususan kiutawala, kiuchumi, kidini, kisiasa na kijamii. Basi, makala hii ililenga kuchunguza jinsi mwandishi wa tamthilia ya *Bembea ya Maisha* (2022) alivyomsawiri mhusika wa jinsia ya kiume katika kazi yake ili kuweka wazi shughuli za ubabedume zilizojengwa katika mila, itikadi na utamaduni wa jamii husika. Data ya makala ilipatikana kwa kuisoma tamthilia teule kisha kuichanganua kwa kutumia Nadharia ya Ubabedume ambayo hulenga kubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume, hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa mhusika wa jinsia ya kiume amesawiriwa kama mtegemezi, mrithi wa mali, ameruhusiwa kupata mtoto nje ya ndoa, haruhusiwi kujishughulisha na kazi za nyumbani, anaitwa gumba kwa kutopata watoto na anayejitwika majukumu yote ya nyumbani. Masuala haya yamekithiri katika jamii za leo. Ikiwa nchi zinazoendelea zitapiga hatua katika maendeleo, basi usawa wa kijinsia unahitaji kutiliwa maanani na jamii zote.

**Istilahi Muhimu:** Usawiri, Mfumo-dume, Taswira, Ubabedume, Jinsia

## UTANGULIZI

Walsh (1997) anasema kuwa uume huhusishwa na uwezo wa mwanamume kuwa na mafanikio kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Mtaalamu huyu anasema kuwa mwanamume hazaliwi na uume kama sehemu ya viungo vyake bali hujengwa na kukuzwa na utamaduni anamokulia. Vilevile, Connell (2000), anashadidia hili kwa kusema kuwa ubabedume hutazamwa kwa njia zaidi ya moja kama vile mahusiano ya kijinsia, ukatili, malezi na hata kazi. Kauli hii imejengeka katika misingi kwamba utamaduni ni dhana muhimu na ni uti wa mgongo katika ujenzi na matumizi yake kutegemea jamii husika kwa vile, kila jamii ina utamaduni wake.

Kulingana na Chafetz (1974) na Doyle (1985) ubabedume ujitokeza katika desturi kwa jumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, kuwa na tajiriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo. Basi, makala haya yalikusudia kubainisha jinsi mwandishi alivyodhihirisha ubabedume katika kumsawiri mhusika wa jinsia ya kiume.

**Wasifu wa Mwandishi Timothy Moriasi Arege**

Kwa mujibu wa Kinuthia (2010), Timothy Arege ni mzaliwa wa Kaunti ya Kisii magharibi mwa Kenya. Alisomea kuko huko kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi, ambapo alijipatia shahada ya B.A. (Kiswahili na Sayansi ya Kijamii). Mnamo mwaka wa 1998 alipata shahada ya Uzamili (MA) katika taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Katika mwaka wa 2013, alipata shahada ya Uzamifu katika chuo chicho hicho. Mwaka wa 2008/2009, Arege alituzwa kuwa msomi bora na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki, Kenya. Vilevile mwaka wa 2011, Arege alishinda Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta mnamo 2009 kwa kazi yake *Kijiba cha Moyo* (2009). Kwa sasa Arege ni mhadhiri wa somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya. Tamthilia zake nyingine ni pamoja na *Chamchela* (2007) na *Mstahiki Meya* (2009) na *Bembea ya Maisha* (2022).

**Muhtasari wa Tamthilia ya** *Bembea ya Maisha*

Tamthilia ya *Bembea ya Maisha* iliandikwa na Timothy Moriasi Arege katika mwaka wa 2022 na kuchapishwa na *Access Publishers Limited* mjini Nairobi. Tamthilia hii inawahusu wahusika wawili Yona na Sara ambao wanawapata watoto wa jinsia ya kike:- Neema na Asna baada ya kutojaliwa kwa miaka kadhaa. Hata hivyo, jamii inamwona asiye na mrithi kwani watoto hawa si wa jinsia ya kiume. Sara anamsaidia Yona kuwasomesha watoto wao. Neema anapata kazi kule mjini na kuwa wa manufaa kwa wazazi wake. Anatumia pesa zake kugharamia matibabu ya mamake na pia kuwakimu wazazi wake. Hatimaye, msimamo wa Yona kuhusu mila na desturi za jamii yake unabadilika na anaanza kumthamini Sara na Neema aliowadhulumu kabla ya mabadiliko hayo.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala hii imetumia nadharia ya ubabedume. Kulingana na Wells na Holland (2001:2), mwasisi wa nadharia hii ni Robert Bly wa Marekani katika mwaka wa 1991. Nadharia hii inajikita katika maumbo ya vitambulishi vya jinsi ya kiume kwa kuzingatia jamii, maandishi na matukio au maelezo ya kihistoria. Isitoshe, mkondo wa nadharia hii unawania kuhalalisha desturi za jinsia ya kiume na ubabedume. Nadharia hii ilitokana na mwamko wa vuguvugu la wanaume ambalo lilichochewa na kazi za Robert Bly na wengine (Chafetz, 1974). Kichocheo cha vuguvugu la wanaume kilitokana na uhakiki wa jinsia ya kiume na utawala wa wanamume unaoathiri kila sehemu ya jinsia ya kike pamoja na mageuzi ya miaka ya 1960. Huu ulikuwa wakati wa upeo wa mgogoro wa itikadi za kijamii katika nchi za Marekani ambazo zilihitaji kuzingatia upya majukumu ya kijinsia. Mgogoro huu ulihusu nafasi na majukumu ya kijinsia katika jamii.

Kulingana na mihimili ya nadharia hii, utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, matukio na maelezo ya kihistoria (Wells na Holland, 2001). Aidha, wanaume wametawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilimali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini (Collins, 1971). Nadharia hii ilifaa katika kuweka wazi masuala yanayodhihirisha vitendo vya ubabedume kupitia kwa wahusika wa jinsia ya kiume.

**Mbinu za Utafiti**

Data ilipatikana kwa tamthilia ya *Bembea ya Maisha* kisha kuzichanganua kwa kufuata lengo la makala na mihimili ya nadharia iliyotumika.

**Matokeo ya Utafiti**

Makala haya yalikusudia kubainisha usawiri wa mhusika wa jinsia ya kiume. Matokeo yamedhihirisha kwamba mwandishi amemchora mwanamume ambaye ana sifa zinazohalalishwa na mila na desturi za jamii ya mwandishi. Sifa hizi ni kama vile: mwanamume ni mtegemezi, mrithi wa mali, ameruhusiwa kupata mtoto nje ya ndoa, haruhusiwi kujishughulisha na kazi za nyumbani, gumba kwa kutopata watoto na anayejitwika majukumu yote ya nyumbani.

**Mwanamume kama Mtegemezi**

Kulingana na Nadharia ya Ubabedume majukumu katika jamii hugawanywa kiuana. Kuna yale ambayo yametengewa jinsia ya kike na mengine jinsia ya kiume. Mgawanyo huu hudhihirisha namna mamlaka na uwezo hugawanywa kijinsia. Mwandishi wa tamthilia husika amemsawiri mwanamume kama mhusika anayemtegemea mwanamke. Yona analalamika kuwa mkewe Sara hajapika chakula hata ingawa ni mgonjwa. Ijapokuwa Yona anayaelewa haya, kulingana na utamaduni wa jamii yake hawezi kumsaidia mkewe ila tu kumtegemea kwa majukumu ya nyumbani. Kwa mfano:

> **Yona**: Sara, bado ungali pale pale? Nyumba hii haifuki walau moshi hata kama chakula ni taabu kwako?
>
> **Sara:** Yona mume wangu, moshi utafukaje? Mwenzio hapa nilipo kichwa kimeudara mto siku nzima. Wewe unajua ni kwa ajili ya maradhi haya, si kwa uzembe wala raha.
>
> **Yona**: Ndipo tufe njaa?
>
> **Sara**: (Akimtazama usoni.) Sivyo…
>
> **Yona**: Ndivyo. Njaa haileti shibe Sara!
>
> **Sara**:…Miaka yote hiyo nikiwa ningali mzima na afya yangu mbona sikufanya ajizi? Muda wote huo nikipika mimi, nikiandaa na kukukaribisha ule. Iweje leo kazi hiyo inishinde? Yalaumu maradhi (Uk 1).

Suluhisho la Sara lawa nikumwita jirani yake Dina aje kumsaidia kupika kwani hawezi kupata usaidizi wa Yona katika kazi za nyumbani. Sara anasema yafuatayo anapoulizwa kama bado nyumba haifuki.

> **Yona**: Hivi leo nyumba hii haifuki?
>
> **Sara**: Subiri. Nimempelekea Dina salamu aje akatufanyie chochote. Mwenzio nilivyo hivi mwenyewe hata sijifai kitu. Mwili mzima mfano wa bua.
>
> **Yona**: Haidhuru. Nitasubiri.
>
> **Sara**: Hatakawia. Yeye huitika wito haraka (uk 4).

Hatimaye, Dina anaitikia wito wa Sara. Anamwambia Kiwa kuwa:

> **Dina**: Mwanangu sasa mimi ninaondoka. Ninaenda kwa Sara kumsaidia na upishi. Hali yake ile haimwezeshi kufanya chochote. Amenitumia salamu niende kumsaidia lakini kwa kuwa nilikuwa nimebandika sufuria, nikaona heri nimalize upishi wangu (uk 11).

Mazungumzo baina ya Dina na Sara yanaashiria kuwa malezi na makuzi ya Yona hayamruhusu kuingia jikoni ili kumfaa mkewe. Yona anaona heri kuondoka nyumbani badala ya kupika ilhali mkewe ni mgonjwa. Wanasema hivi:

> **Sara**: Ninajua sasa karibu arudi.
> **Dina**: (Anaanza kupika.) Hivi amekwenda wapi?
> **Sara**: Hakusema. Ameondoka tu. Alikuwa amekuja kutoka huko kwa wenziwe kupata chochote lakini akapata mwenyewe nilivyo hoi hata jiko halijaona kiberiti. Ilivyo desturi ya wanaume wetu, naye akataka kujua kwa nini sikumwandalia chochote.
> **Dina**: Haoni hali yako?
> **Sara**: Anaona lakini ninafikiri malezi na makuzi yanamtuma hivyo.
> **Dina**: Wanaume wetu hawa! Hawawezi hata kusaidia kupiga makasia chombo kinapopungukiwa upepo! (Uk 13-14).

**Mwanamume kama mrithi wa mali**

Wells na Holland (2001:16) wanadai kuwa nadharia ya ubabedume inawania kuhalalisha desturi za jinsia ya kiume na ubabedume. Wanajamii wanaunga hoja hii wanaposhikilia kuwa mtoto wa kiume ndiye hurithi fimbo ya baba. Mazungumzo baina ya Yona na Sara yanaangazia haya wanaposema yafuatayo:-

> **Yona**: …Sharti ujue kwamba fimbo ya mzee hurithi mtoto wa kwanza.
> **Sara**: Fimbo wanarithi watoto wa kiume; si wa kike (uk 2).

Mfumo dume huu unaungwa mkono na wanawake wenyewe kama Sara anavyosema.
Yona amejaliwa watoto wa jinsia ya kike kumaanisha kuwa hana mrithi kama vile Sara anavyosema.

Jamii nayo inaunga mkono kauli hii kama anavyosema Dina kwa Kiwa.

> **Dina**: Lakini kama ujuavyo mwanangu mwanadamu sawa na tumbo, hakinai.
> **Kiwa**: Hivi kweli mama tumbo halikinai?
> **Dina: …**Roho ndiyo hukinai.
> **Dina**: …hayakuishia hapo. Baada ya ile mvua ya baraka iliyowanyea, watu walianza tena kuwasema kuwa hawana mtoto wa kiume.
> **Kiwa**: Kwa nini hilo nalo liwakere:
> **Dina**: Mahasidi hawana sababu. Halafu upo huo Uafrika mwanangu. Watu waliuliza na wangali wanauliza ardhi ya Yona atarithi nani! (uk 8).

Ni wazi kwamba jamii inamthamini mtoto wa jinsi ya kiume kumliko wa kike. Imani ikiwa wa jinsia ya kike ataolewa na kumwacha mzazi wake. Imani hii inamdhalilisha mtoto wa jinsia ya kike na kumpa nafasi ya juu yule wa kiume.

Wazee wenzake Yona walimhimiza kumwoa mke mwingine ili amzalie mtoto wa kiume ambaye angekuwa mrithi wake. Dina anasema hivi: -

> **Dina**: Nilikuwa nimesahau. Naam, hazikwisha kamwe. Watu walimtia Yona maneno kuwa lazima awe na mrithi. Walimtaka aoe mke atakayemzalia watoto wa kiume kwa kuwa, kwa maneno yao, Sara alikuwa ameshindwa.
> **Kiwa**: Kweli?
> **Dina**: Sijui imekuwaje lakini haikupata kutokea hivyo licha ya minong'ono yote iliyokuwepo. Ila unyanyapaa ulimfanya Yona kuupokea ulevi kwa mikono miwili (uk 9).

Dondoo hili linaashiria kuwa mwanamume akosapo mtoto katika ndoa, mwanamke ndiye hulaumiwa.

Dina anamfahamisha Kiwa kuwa Sara alipokea kichapo kwa kutomzalia Yona mtoto wa kiume. Hatimaye, kichapo hiki kilimsababishia maradhi ya moyo.

> **Dina**: Hao wametoka mbali. Upo wakati hakuna aliyeamini wangeishi pamoja. Pamoja na ulevi wake, Yona alianza kumpiga Sara; tena kipigo cha mbwa hasa alipokuwa amelewa. Mara kadhaa alimwagiwa maji baridi kumrejeshea fahamu.
> **Kiwa**: Kwa nini kichapo chote hicho?
> **Dina**: Eti hakumzalia mtoto wa kiume (Uk 10).

Jamii ya Kiafrika ina Imani kuwa iwapo familia haina mtoto wa jinsia ya kiume basi haina mrithi yeyote.

**Mwanamume ameruhusiwa kumpata Mtoto nje ya Ndoa**

Kulingana na nadharia ya ubabedume, kunazo sifa angama za uwezo-uume ambazo ni sharti mwanamume awe nazo ili kuweza kujenga, kudumisha na kudhihirisha ubabe. Sifa hizi ni kama vile; uvumilivu, uwezo, kutoogopa, kuthubutu, ukware miongoni mwa sifa nyingine. Makala hii imepata kwamba jamii inamsukumwa Yona kuwa mkware ili kuthibitisha ubabedume wake. Sara anapomzalia Yona watoto wa jinsia ya kike, rafikize walimshauri aoe mke mwingine ambaye angemzalia watoto wa kiume kwani Sara alikuwa ameshindwa. Kauli hizi zilikuwa zikimwelekeza kuwa mkware. Dina anamwambia Kiwa yafuatayo:

> **Kiwa:** Ulikuwa unasema karo za watu hazikuishia pale.
>
> **Dina**: Nilikuwa nimesahau. Naam, hazikwisha kamwe. Watu walimtia Yona maneno kuwa lazima awe na mrithi. Walimtaka aoe mke atakayemzalia watoto wa kiume kwa kuwa, kwa maneno yao, Sara alikuwa ameshindwa (uk 9).

Rafikize Yona wanapendekeza kwamba atafute mtoto nje ya ndoa mradi awe wa kiume ili athibitishe kuwa ana ubabedume. Wanaamini kwamba atakuwa amepata mrithi na jina lake halitapotea. Haya yanafanyika ilhali Yona ana watoto wawili; Neema na Asna walio wa jinsia ya kike. Jamii haithamini watoto wa jinsia ya kike basi inachangia katika kuendeleza ubabedume. Shinikizo hili linamfanya Yona kuingia katika ulevi. Dina anamwambia Kiwa kuwa:-

> **Dina**: Ninakwambia kwa mikono yote miwili. Wewe umekua ukampataYona kipenzi cha maji. Hakuwa hivyo.
>
> **Kiwa**: Alaa!
>
> **Dina**: Alisukumwa huko na wimbi la maneno ya watu. Wengine wakamsukuma kutafuta mtoto huko nje kwa kila hali mradi awe wa kiume. Amrithi yeye. Eti jina lake lisipotee. Utambi wa ukoo wake usizime (uk 10).

Kwa hakika, jamii inachangia katika kumfanya mwanamume kufanya juu chini ili kuthibithisha nguvu zake za uume hata ingawa amezalisha kiumbe mwanamke.

**Mwanamume Haruhusiwi Kujishughulisha na Kazi za Nyumbani**

Sara anamwelezea Dina kuwa mila na desturi za jamii yao zimemkuza mwanamume kuwa kuna kazi za wanawake na za wanaume. Ni makosa kwa mwanamume kuingia jikoni. Isitoshe, iwapo atamsaidia mkewe, watu watasema kuwa amedhalilishwa. Sara anamwambia Dina: -

> **Dina**: Wakati mwingine ninashindwa kuwaelewa.
>
> **Sara**: Wenyewe tumewafanya hivyo. Mila na desturi zetu zimewajenga hivyo walivyo na sisi hivi tulivyo. Kazi zote za nyumbani ni zetu. Yaani kwake mtu lakini hajui hata chumvi inakowekwa. (Wanacheka.). Yeye anajua sebuleni, msalani na chumba cha kulala. Haya yasiyotarajiwa yajapo tayari mtu ana kilema kikubwa japo mzima viungo vyote. Anaishi kuwa mgeni wa mambo mengi kwake nyumbani. Tutafanya nini? Wenyewe tutasukuma vivyo hivyo (Uk 14).
>
> **Dina**: Sijui tufanye nini.
>
> **Sara**: Utafanya nini mwenzangu? Dunia ikijua anakusaidia jikoni itasema unashusha hadhi yake na kwa mizani ya jamii utakuwa unajivulia nguo (Uk 14).

Kutokana na mazungumzo ya Sara na Dina, ni wazi kuwa utamaduni wa jamii hii umejikita katika imani na desturi ambazo zimetamalaki katika mfumo mzima wa jamii.

Sara anashauriwa na Asna pamoja na Neema akae mjini ili apate matibabu kisha apumzike lakini anadai kuwa amemwacha Yona pweke nyumbani. Kazi za nyumbani kama vile kushughulikia kuku asubuhi kisha mbuzi na ng’ombe, kujipikia kiamshakinywa na kuendea maji kisimani zitamlemea. Baadaye, kijiji kizima kitamtazama Yona kwa jicho la dharau kwani kazi kama hizo ni za mkewe.

> **Asna**: Baba bado kijana. Hawezi kushindwa kuteka maji kisimani.
>
> **Sara**: (*Kwa ukali.*) Hivi mtoto una akili wewe? Babako aende kuteka maji kisimani? Wazee wenziwe watamwonaje? Kijiji kitasema nini? Kwamba amesomesha watoto ambao wameniweka jijini ili baba yao ataabike? Watu wapate sababu ya kumtazama kwa sini ya dharau? Hmm! Hiyo ndiyo heshima? (uk 44-45).

Dondoo hii inathibitisha kwamba kazi ya nyumbani ni za wanawake pekee. Wanaume hawapaswi kujishughulisha nazo kamwe.

Hata ingawa Beni aliye mzee mwenzake Yona anaelewa kuwa Sara yuko mjini kwa matibabu, analalamika kuwa Yona ameachwa pweke ili ajipikie.

> **Luka**: … Mtu kupata matibabu au kuja kumpikia mwenzake?

**Beni**: Yona, muda wote uliokaa nani anakupikia mzee mwenzetu? Hii ni miaka ya kujipikia? Ningeelewa zamani zile ukiwa mwalimu kabla ufutwe kazi. Siku zile ulikuwa na nguvu zako. Sasa misuli yako imenyauka (uk 61).

**Mwanamume anaitwa Gumba kwa Kutopata Watoto**

Nadharia ya Ubabe-Dume inataja kwamba kuna sifa angama za uwezo-uume ambazo ni sharti mwanamume awe nazo ili kuweza kujenga, kudumisha na kudhihirisha ubabe. Sifa hizi ni kama vile; uvumilivu, uwezo, kutoogopa, kuthubutu, ukware miongoni mwa sifa nyingine. Kulingana na tamthilia hii, mwandishi kwa kupitia mazungumzo ya Dina na Kiwa inaweka wazi kwamba ubabe dume wa Yona ulitiliwa shaka na jamii kwa kusema kuwa na watoto katika ndoa yake na Sara. Dina anamwambia Kiwa kuwa:-

**Dina**: Mwanangu nikwambie nini? (Kimya.) Sara ameitwa tasa. Wakati mwingine yeye na mumewe wameitwa wagumba, japo shoka la ugumba limemwangukia yeye zaidi kuliko mwenziwe.
**Kiwa**: Lakini mama, si wana watoto? Au ndiyo unasema watoto hawa si wao?
**Dina**: Damu yao hiyo lakini wameiona baada ya hodari wa kusema kuwabandika hili na lile.
**Kiwa**: Vipi hivyo?
**Dina**: Yaani yamesemwa mengi siku nyingi kama ilivyo ada katika jamii nyingi za Kiafrika… Kwa ufupi, Yona alifunga uchumba na Sara na hatimaye wakaoana na kuishhi vizuri ila milango ya baraka ya watoto ikakawia kufunguka. Tulivyo Waafrika, ikawa kuna waliolijua tatizo kuliko wenye tatizo. Kazi ikawa ni kuwasema, wakalaumiwa na kusutwa. …Lakini hatimaye Mungu akaridhia wakati wake aliouona bora (Uk 7).

Haya yanaashiria kwamba, jamii inamwona mwanamume asiye na watoto katika ndoa kuwa mwanamume asiyekamilika.

Sara anawaambia watoto wake Neema na Asna kuwa yeye na Yona walichukua muda kabla ya kuzaliwa mtoto. Jamii iliwalaumu na hata walipowapata kina Neema na Asna bado walionekana maskini wa mrithi. Anamwambia Asna:-

**Sara**: Tulikosa mengi. Kwanza sisi wazazi wenu tulichukua muda kabla ya kujaliwa mtoto. Watu walituona maskini wa watoto. Maskini wa kizazi…Tulipofarijika kwa kumpata Neema na nyinyi mkafuata, bado wakatuona maskini wa mrithi. Maskini wa kushikwa mkono uzeeni…Hatimaye wengine walitutenga lakini kwa kudura za Mungu jahazi halikuzama (Uk 55).

**Mwanamume amejitwika Majukumu yote ya Nyumbani**

Chafetz (1974) na Doyle (1985) wanasema kuwa maeneo ya ubabedume yanajitokeza katika desturi kwa jumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, kuwa na tajiriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo. Katika jamii za Kiafrika, majukumu hugawanywa kiuana. Kuna yale ambayo yametengewa jinsia ya kike na mengine jinsia ya kiume. Mgawanyo huu hudhihirisha namna mamlaka na uwezo hugawanywa kijinsia. Utamaduni wa jamii hujikita katika imani kuwa majukumu ya nyumbani hujitwika mwanamume. Yeye sharti aifae familia yake katika mahitaji ya kimsingi ambayo ni mavazi, nyumba, chakula na elimu. Bunju anamwambia Neema kuwa ni wajibu wake (Bunju) kukidhi mahitaji ya familia yake bila kumhusisha.

**Bunju**: Ema, unafahamu vizuri kuwa nimechukua mkopo wa benki kujengea nyumba hii. Mkopo huo haunipi amani. Ninahangaika kuulipa. Wewe mwenyewe ulikazana kwamba Mina aende *boarding school*. Tena shule ya gharama. Pesa nyingine nitatoa wapi?
**Neema:** Buu, mtoto wa kwanza anafaa kusomea shule ambayo inatia matumaini. Fahari iliyoje mtoto kusomea shule ambayo haikupi wasiwasi!
**Bunju**: Mimi wajibu wangu kwenu ninautimiza. Je, sinunui chakula?
**Neema**: Unanunua bila shaka.
**Bunju**: Mavazi?
**Neema**: Tunayo.
**Bunju**: Si hivi majuzi nimekununulia gari?
**Neema:**…
**Bunju**: …Mimi nilikwisha kukueleza kuwa mzigo wa familia yangu unatosha kunishughulisha (Uk 27).

Bunju anafahamu fika kuwa ni jukumu lake kama mwanamume kukidhi mahitaji ya familia yake bila kumhusisha Neema. Anamwambia Neema kuwa ana uhuru wa kutumia mshahara wake ili kulipia matibabu ya mamake. Bunju amemnunulia gari na ni wajibu wake kuinunulia mafuta. Anamwambia Neema haya:

**Bunju:** Shukuru una mahali pa kuamkia siku baada ya siku. Bila hapo ungekuwa unajipa shughuli gani?

**Neema**: Daima ninashukuru japo hakitoshi.

**Bunju**: Hakitoshi vipi?

**Neema**: Mahitaji yenyewe ni mengi.

**Bunju**: Sielewi. Nyumba ni juu yangu, karo ninalipa mimi, chakula ninanunua mimi, matibabu vilevile ni juu yangu. Sasa wewe mshahara wako huo mbona usitoshe? Mafuta ya gari ndiyo yanaumaliza?

**Bunju**: Wajibu wangu kama mume nitafanya na nimejitolea kutekeleza kwa hali na mali kufikia hapo. Wewe unajua uzito wa majukumu niliyo nayo. Mshahara wako sikuombi wala sikupangii. Gharama zote zinaujua tu mfuko wangu (uk 39-40).

Mazungumzo baina ya Bunju na Neema yanaashiria kuwa ni jukumu la mwanamume kukidhi mahitaji yote ya familia yake. Jamii inatarajia kwamba mkewe hatahusishwa kwa vyovyote vile. Kutekeleza majukumu haya ni ishara tosha kuwa mfumo dume umemwekea mwanamume masharti hayo.

## HITIMISHO

Makala hii imebainisha kuwa kunao ubabedume uanodhihirika katika jamii kupitia kwa wahusika waliotumiwa na mwandishi. Mhusika wa jinsia ya kiume amesawiriwa kama mtegemezi, mrithi wa mali, ameruhusiwa kupata mtoto nje ya ndoa, haruhusiwi kujishughulisha na kazi za nyumbani, anaitwa gumba kwa kutopata watoto na anayejitwika majukumu yote ya nyumbani.

## MAREJELEO


Chafetz, J. (1974). *Masculine / feminine or human*? Itasca, IL: Peacock Publishers.

Collins, R. (1971). A Conflict Theory of Sexual Stratification. In *Social Problems*19,3-21.https://doi.org/10.1525/sp.1971.19.1.03a00010. Accessed on 26th October 2022.

Connell, R. 2000.*The Men and the Boys.* Sydney, Allen & Unwin; Cambridge, Polity Press; Berkeley, University of California Press**.**http://www.raewynconnell.net/p/masculinities_20.html Accessed on 26th October 2022.

Doyle, J.A. (1985) Sex *and Gender.* Iowa: CW Brown Publishers.

Kinuthia, K. (2010). Kumhusu mwandishi Timothy Arege. Moi U niversity. https://www.coursehero.com/file/p1fq55t/Kumhusu-mwandishi-Timothy-Arege-Timothy-Arege-ni-mzaliwa-wa- Kaunti-ya-Kisii/. Ilichukuliwa 25/10/2022.

Omari, S. (2008), Fasihi Simulizi na Jinsia. Katika *Kiswahili Juzuu ya 71(71),* Dar es Salaam: TUKI. Retrieved on 21st O ctober 2022

Walsh, M. R. (1997). *Women, Men and Gender: Ongoing Debates*. London: Yale University Press, New Haven. Wells-Wilbon, R. na Holland, S (2001). Social Learning Theory and the Influence of Male role models on African American children in PROJECT 2000. The Qualitative Report 6(4). (July 2 7th2007) http://www.nova.edu/ssss/QR/QR6-4/wellswilbon.html. Accessed on 27th October 2022.